

Ukombozi (Redemption)

by

Jeremiah Zablon

Ukombozi (Redemption)

by

Jeremiah Zablon

December 11, 2012

Ukombozi

Neno ukumbozi hapa linamanisha gharama ya kununua kwa uhuru wa mwingine kutoka utumwani. Biblia inatuambia jinsi Mungu alivyo wakomboa wana wa Israeli kutoka katika utumwa wao Misri. (Kut. 6:6). Tunaambiwa kwamba kulikuwa na sheria iliyofuatwa ili mtu aweze kutimiza masharti ya ukombozi (Law. 25:23-34). Katika Agano la Kale, Sheria ilihitaji kwamba Waisraeli watoe dhabihu kama sheria ya kale ili mtu aweze kutimiza masharti ya ukombozi (Kut. 12. Isaya anatuambia kwamba, Mungu hakupendezwa na dhabihu walizotoa Waisraeli kwa wakati ule (Isa. 1:11). Mungu aliwaambia kwamba, “*nimechoka na sadaka za kuteketezwa za mbuzi wanene na ng’ombe, sifurahii damu za ng’ombe na wana mbuzi au kondoo.*” Katika sehemu nyingine, Yereimia anasema, “*Angalia siku zinakuja asema BWANA nitakapofanya agano jipya na nyumba ya Israeli, na nyumba ya Yuda.*” (Yer. 31:31).

Kulipaswa kuwa na mabadiliko katika sheria ya ukombozi kama katika Sheria zingine ambazo Mungu aliwapa wana wa Israeli ijulikanayo kama sheria kumi (Kut. 12). Kama Mungu alivoahidi kuleta mabadiliko na mkombozi, Mungu mwenyewe ndiye alikuwa mkombozi (Isa. 63:16). Katika Agano Jipya tunasoma kwamba Simoni akitoa ushahidi wa Yesu kama Mkombozi (Luka 2:28). Huu ulikuwa ni ukombozi wa kiroho.

Leo watu wamewekeza katika njia zaao wenyewe ya kuwaokoa rafiki zao kutoka katika utumwa wa dhambi; wengine wanaomba kwa kuwasha mishumaa miekundu, kujani, nyeupe, na blu; wengine hata wanafunika dhambi hizo na nguo nyekundu, kijani, na blu, na wengine bado wanatoa dhabihu ya wanambuzi, mbuzi, na ng’ombe; yote haya na matendo mengine ya ukombozi wanaifanya kwa jina la Yesu, wakati yote haya ni matendo potofu ya ukombozi.

Neno ukombozi hapa inamanisha kwamba Yesu kama Mwana kondoo aliuawa ili kumnunua mwenye dhambi aje kwa Mungu kwa damu ya wanyama lakini damu yake mwenyewe huwaokoa wanadamu wa kila kabila na lugha, na watu, na taifa (Ufu. 5:9). Yohana anatuambia kwamba siku iliyofuata alimuona Yesu akimwendea na kusema, “*Tazama Mwana kondoo wa Mungu aondoaye dhambi ya ulimwengu.*” (Yoh. 1:29; Ufu. 5:6). Leo ni vyema kwa kila mtu ambaye angependa kuja katika uhusiano na Kristo kufahamu kwamba Kristo pekee ndiye girantii ya urithi wetu (Efe. 1:14). Hiyo inamanisha kwamba ukombozi uko tu ndani ya Kristo kwa dhabihu ya damu yake (Efe. 1: 7). Luka katika Mdo. 4:12 anatuambia kwamba hakuna jina lingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu tuwezalo kuokolewa kwalo. Hiyo

inamanisha mtu lazima awe na uhusiano na Kristo ili kuwa na ukombozi na msamaha wa dhambi (Rum. 6:3; Kol. 2:12).

Katika vifungu hivi viwili, ubatizo ndio njia pekee ya tendo la muitikio sehemu ya mwenye dhambi anayekubali zawadi ya bure ya neema pasipo masharti, ambayo ndio gharama ya kumuokoa mwenye dhambi.

Ukombozi uko katika Kristo, ni bure kwa neema yake (Rum. 3:24). Katika msitari huu neema inamanisha upendo wa upendeleo wa Mungu ambao alipewa mwanadamu mwenye dhambi bila kujali hali ya kiroho ya wanadamu wote. Paulo anatuambia kwamba tulipokuwa tungali wenye dhambi Kristo alitufia (Rum. 5:8). Mungu anampango wa kuwaokoa wanadamu wote kutoka dhambini na ghasia ya dhambi (Zab. 72:14). Katika Efe. 1:7 paulo anatumia neno ukombozi kuelezea ununuzi wetu kutoka katika hali ambayo tusingeweza kutoka wenyewe kwa matendo ya Sheria au matendo ya urithi (Kol. 1:14). Ndugu tunapaswa kutambua kwamba Yesu ametukomboha kutoka dhambini, hiyo ambayo tusingeweza kutoka wenyewe. Leo watu wote wanapaswa kutambua kwamba kuna ukombozi kutoka katika ghadhabu ya Yesu Kristo (Rum. 6:23; Rum. 8:1). Hivyo twende nje na kuhubiri injili ya Yesu kwa watu wote katika mataifa yote kama agizo la Yesu (Mat. 28:18-19).

Mungu awabariki mnaposoma jarida hili.

Na Jeremiah Haudu Zablon

Nakuru, Kenya

